

HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI

MUHTASARI WA KIKAO CHA WAKUU WA IDARA NA VITENGO (CMT)

KWENDA KWA: WAKUU WA IDARA NA VITENGO

KUTOKA KWA: AFISA UTUMISHI NA UTAWALA (W)

Kumb Na: AJ.81/177/321/94

YAH: MAMBO YA KUFANYIA KAZI KUFUATIA KIKAO CHA CMT CHA TAREHE 09/11/2021.

MAHUDHURIO:

A: WATAALAMU WALIOHUDHURIA: KIKAO CHA CMT CHA TAREHE 09/11/2021.

- | | |
|----------------------------|----------------------------------|
| 1. Bw. Bw. Denis Kitali | -Kaimu Mkurugenzi Mtendaji(W) |
| 2. Bw. Sudi S. Khassim | -Kaimu Afisa Utumishi(W) |
| 3. Bw. Nadhiri S. Khamis | -Kaimu Mganga Mkuu (W) |
| 4. Bi Rehema Issaay | -Mwekahazina |
| 5. Bw. Tumainiel Kamnde | -Afisa Manunuzi |
| 6. Bw. Damian Mnenwa | - Kaimu Afisa Mipango |
| 7. Bw. Anthony Nyange | -Afisa Maendeleo ya Jamii |
| 8. Bw. Conrad Ntibandebage | -Afisa TEHAMA (W) |
| 9. Bw. Bwenda I.Bainga | - AfisaKilimo, Umwagiliaji(W) |
| 10. Bw. Jamali Saidi | -Afisa TASAF |
| 11. Bw. Jafet Manyama | -Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W) |
| 12. Bw. Richard Mwalonde | -Mkaguzi wa ndani (W) |
| 13. Bw. Swalehe Njoma | -Mwanasheria (W) |
| 14. Eng. Jacob Mwakyambiki | -Mhandisi Ujenzi(W) |
| 15. Bw. Hamad Mgaluli | -Afisa nyuki(W) |
| 16. Bi. Asha Mungia | - Afisa Elimu Sekondari |
| 17. Bw. Laban Kitule | -Kaimu Afisa Mazingira |
| 18. Bw. Mahodha Kizima | - Kaimu Afisa Elimu Msingi |

B. WATAALAM WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA

- | | |
|--------------------------|-------------------------|
| 1. Bw. Mohamed I. Mavura | -Mkurugenzi Mtendaji(W) |
|--------------------------|-------------------------|

C: SEKRETARIET.

- | | |
|----------------------|---------------------|
| 1. Bi. Raya T. Mlawa | -Mwandishi wa Vikao |
| 2. Bw. Mao Kasanga | -Mwandishi wa Vikao |

AGENDA NA. 01: KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti baada ya kusalimia wajumbe na kuwakaribisha kikaoni, Alieleza kuwa hiki ni kikao cha wakuu wa idara na vitengo ambacho kinajadili shughuli zinazotekelezwa kwenye idara zao na kuwataka wajumbe kuwa makini kujadili ili kutoka na maazimio ya pamoja.

Baada ya maelezo hayo alifungua kikao saa 02:09 Asubuhi.

AGENDA NA. 02: KURIDHIA AGENDA ZA KIKAO.

Jumla ya agenda kumi (10) ziliwasilishwa kikaoni ili zijadiliwe nazo ni;

1. Kufungua Kikao.
2. Kuridhia Agenda.
3. Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa tarehe 09/11/2021.
4. Yatokanayo na kikao cha CMT cha tarehe 09/11/2021
5. Taarifa ya Mapato ya Wiki kuanzia tarehe 01/11/2021 Hadi 07/11/2021
6. Taarifa ya DEFAULTER's
7. Mapendekezo ya Mchoro wa Mipango miji
8. Taarifa ya Mapokezi ya fedha kiasi cha **Tshs. 1,480,000,000.00** kwaajili ya Ujenzi wa Madarasa 8 Shule Shikizi pamoja na ujenzi wa Madarasa 51 Shule ya Sekondari.
9. Taarifa za Utekelezaji wa Kazi za Idara.
10. Kufunga kikao.

Baada ya agenda hizo kupitiwa Wajumbe wote kwa pamoja waliridhia agenda zote kumi (10) Kujadiliwa.

AGENDA NA. 08: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSHS. 1,480,000,000.00 KWAAJILI YA UJENZI WA MADARASA 8 SHULE SHIKIZI PAMOJA NA UJENZI WA MADARASA 51 SHULE YA SEKONDARI.

Kwa idhini ya Mwenyekiti Mweka hazina aliwasilisha taarifa ya Mapokezi ya fedha kama ifuatavyo;-

Ilielezwa kuwa Halmashauri imepokea fedha

- a) kiasi cha **Tshs. 460,000,000** kwaajili ya ujenzi wa madarasa 23 ya shule shikizi 8 ambazo ni Nyambele, Mweyubaruti, Zimbwini, Usimbe, Kimbendu, Nyambangala, Beta na ndungutu.
- b) Kiasi cha fedha **Tshs. 1,020,000,000** kwaajili ya Ujenzi wa Madarasa ya Shule za Sekondari 12 ambazo ni;- Ruaruke Sec, Mtanga Delta Sec,

Mtawanya Sec, Mahege Sec, Kikale Sec, Mjawa Sec, Mlanzi Sec, Zimbwini Sec, Msafiri Sec, Dimani Sec, Nyamisati Sec na Mchukwi Sec.
Ambapo jumla ya fedha hizo ni Tshs. 1,480,000,000.00

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa Ilisisitizwa Kamati ya Ujenzi ya Wataalam kutembelea maeneo ambayo yanahistoria ya kupata mafuriko ya kata ya Mtunda, Beta na Nyambele ili kujiridhisha kabla ya kufanya maamuzi ya kufanya Ujenzi, katika ziara hiyo Diwani wa Kata ametakiwa kushirikishwa.

Ilielekezwa Mwanasheria kuandaa barua kwa ajili ya kuwaita Watendaji wa Kata zote zilizopata fedha za mradi wa Covid-19, Maafisa Elimu Kata na Wahe. Madiwani wa Kata zilizopatiwa Mradi ili kuja kuwapa maelekezo ya kusimamia fedha za ujenzi wanazoletewa.

Ilielezwa Afisa Mipango kuandaa orodha ya Walezi wa Kata kwa Wakuu wa Idara wote na baadhi ya wasaidizi ili kusimamia Shughuli za ujenzi zinazoendelea kwenye Kata hizo.

Baada ya Mjadala huo Wajumbe wote kwa pamoja waliridhia na maelekezo hayo kuendelea kufanyiwa kazi.

AGENDA NA 10: KUFUNGA KIKAO.

Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe kwa miachango yao na kuisitiza yaliyoagizwa yakafanyiwe kazi. Baada ya maelezo hayo alifunga kikao saa 04:45 Asubuhi.

MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA;

Ditaki
.....

SAINI YA MWENYEKITI

DENIS KITALI
.....

JINA LA MWENYEKITI

09/11/2021
.....

TAREHE

[Signature]
.....

SAINI YA KATIBU

SUD S.K
.....

JINA LA KATIBU

09/11/2021
.....

TAREHE